**MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI DOGO LA KANGEMA– 2016**
**KISWAHILI**
**102/3**
**KARATASI YA TATU**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1.** Ushairi
a) Sodoma na Gomora Uozo
Ouvu katika jamii *1 x 1 = 1*
b) Mathnawi - vipande viwili T
arbia - mishororo minne
Ukaraguni - vina kutofautiana katika kila
Ubeti *3 x 1 = 3*
c) Nidaa - oie wangu
Takriri - ole wangu, ole wangu
Istiari - nyakati zinalinganishwa na
Sodoma na Gomora
*3 x 1 = 3*
d) Ritifaa
Ka - badala ya kama - kupata urari va
Mizani
*1 x 2 = 2*
e) Tabdila - walipuao - walipuayo Kuleta urari wa vina
Kuboranga sarufi - Huruma wamekaidi kupata urari wa vina *1 x 2 = 2*
f) Watu wengine wanataka kuoa watu wa jinsia yao
Eti jinsia tofauti haifai Wanahiari kuoa jinsia yao. Haya ni maoni potovu tupasavyo kuyafaa kwani nyakati tunazoishi zimejaa uovu / dhambi tele ***alama*** *4 x 1*
g) Tamaa
Kutozingatia sheria za Mungu
f) Wizi
g) Uongo
h) Ushirikina *3 x 1 = 3*
h) Masikitiko
Malalamiko *2 x 1 = 2*

**Mstahiki Meya**
**2.**
a) Maneno ya Meya kwa Bili wakiwa ofisini
mwake. Bili alimwelezea Meya jinsi watoto wake walivyofurahi baada ya kujistarehesha kajifahari *4 x 1 = 4*
b) Balagha - mbona isiwe kweli ?
Istiara - matunda ya jasho letu
Kinaya - wanacheneo ndio hutoa jasho ila meya asema ni jasho lao *2 x 1 = 2*
c )
- Meya anamweieza Bili kuhusu mwanakandarasi aliyetaka kuendelea na kazi
i) Meya aliogopa kusitisha kandarasi yake ili asishtakiwe
j) Bili anashauri Meya asitishe ndipo mwanakandarasi aende kortini
k) Itaamriwa apate thamani ya pato lake
l) Anashauri kuwa Meya akubali kuwa alifanya maamuzi kwa niaba ya baraza
m) Baraza ndilo litakalolipa
n) Kwamba akubaliane na mwanakandarasi kuhusu fungu atakalopata haada ya mwanakandarasi kulipwa
*7 x 2 = 14*

**3.** Maudhui ya unafiki
- Meya anajifanya kuwa kiongozi wa kupigiwa mfano ilhali anajinufaisha kwa kujilimbikizia mali kwa njia haramu
- Anatoa maneno ya kumnasa mhubiri. Hataki sura ya baraza kuathirika kwa njia yoyote ili afaidi misaada kutoka kwa wageni,
- Bili anajifanya rafiki wa Meya na kumbe ajenda yake ni kujinufaisha na mambo yanapoharibika anatoweka Diwani I alijifanya mzuri ili achaguliwe na alipopata cheo akawageuka na kuanza kuwatesa kwa mashambulizi
- Diwani **II** baada ya kuchaguliwa anakuwa kiini cha propaganda zinazosambazwa na vyombo vya habari
- Mhubiri ni mnafiki kwani anayafahamu madhila yanayowakumba wanacheneo lakini anaomba uongozi wa Meya udumu
- Mhazili anajifanya mtumishi mzuri wa Meya lakini anamsaliti Meya kwa kushiriki katika mgomo
- Dida anajifanya mpole, mnyenyekevu na baadaye anamdhihaki Meya kwa kuigiza jinsi Meya huwatusi na kutowaheshimu wafanyikazi wake Wahusika *5 x 4 = 20*

**4.** a)
i) Maneno haya yalisemwa na Dora

ii) Msemewa ni Majisifu
iii) Walikuwa nyumbani mwao
iv) Majisifu alikuwa anataka kuwatupa watoto waliozaliwa majini kwa kuwa hawakuwa na uv/ezo wa kutembea lakini Dora akamzuia *4 x 1 = 4*

b) Methali - mtu hupata ajaliwalo sio alitakalo
Istiara - likiwa bonge la nyama *1 x 2*

c)
- Imani alikuwa na ndoto ya kuwa daktarii lakini anakosa kusoma na kuishia kuwa kijakazi
- Nasaba Bora alikuwa na Imani kuwa mazishi yake yangehudhuriwa na wengi lakini baada ya kifo chake mazishi yalihudhuriwa na wachache mno
- Majisifu alitamani kupata watoto wazima kama wenzake badala yake watoto wake wanazaliwa wakiwa vilema
- Mashaka alisema badala ya Mungu kumpa kilema chochote afadhali ampe kifo. Hata hivyo anaishia kuwa kichaa
- Nasaba Bora alitarajia madhubuti aweze kuendeleza kazi yake lakini madhubuti anamgeuka na kuwa hasidi wake
- vi Bi Zuhura alitamani kupata mapenzi kutoka kwa mumewe lakini anachopata ni upweke na majonzi na hatimaye kupewa talaka
- Amani licha ya kusoma hadi chuo kikuu anasingiziwa uchochezi na kutokamilisha masomo yake hapati umaarufii wowote. Badala yake Majisifu anapata Sifa kemkem huku Amani akiwa mchungaji ***7x2 = 14***

5.

- Unyakuzi wa ardhi - Nasaba Bora anabadilisha hatimiliki ya shamba la chichiri Hamadi
- Mauaji - Nasaba Bora anapanga njama Chichiri Hamadi auawe
- Umaskini- Imani anakosa kuendelea na masomo kwa ukosefu wa pesa
- Matumizi mabaya ya pesa za umma - Nasaba Bora na washirika wake wanatumia pesa zilizonuiwa kujengea hospitali na kuishia kujenga zahanati
- Huduma duni za afya - nduguye Imani anakufa kutokana na utepetevu wa madaktari / uhuru
- Umma kulazimishwa kumchangia Madhubuti ili aende akasomee Urusi
- Kufungwa jela bila. sababu - Amani na Imani / Yusufu, Matuko Weye
- Maskini kunyimwa nafasi za masomo huku pesa zikiwaendea watoto wa matajiri k.m.
- Fao kufadhiliwa kwa pesa za mahawinde
- Viongozi kama Nasaba kuwa na uhusiano na watoto wa shule kama vile Lowela
- Udangan yifu katika mtihani. Fao anafanyiwa mtihani
- Wiziwa miswaada - mwalimu Majisifu anaiiba miswaada na kuichapisha kwa jina lake
- Kutowajibika - Majisifu hafiki shuleni ***zozote 10 x2 = 20***

6) a) Haya ni maelezo ya mwandishi
o) Anawarejelea Sela na wasichana wengine wawili waliokuwa wameitwa na Bi Margaret
p) Walikuwa katika chumba cha mapokezi
q) Walikuwa wameitwa na Bi Margaret walipokuwa gwarideni na kuwataka wafike ofisini mwake
***4x1 = 4***

b) Istiara - mpango ulikuwa usiku wa giza ***1x2 = 2***

c)
- i) Sela alifukuzwa shuleni na Bi Margaret kuwataka wazazi wake kumtafutia shule mbadala
- Sela alikosa utulivu masomoni alipogunduliwa kuwa alikuwa na ujauzito
- Sela na wenzake waliaibika si haba majina yao yaliposomwa gwarideni
- Sela na mamake walifukuzwa nyumbani na mzee Butali na kukaa na jamaa zao kwa
- majuma matatu
- Sela alilazimika kukaa nyumbani kwa miezi mitatu akikitunza kitoto kisha kurejea shuleni
- Masazu alikosa makini masomoni na hakuendeleza elimu yake baada ya kidato cha nne na kuambulia tu kazi ya vibarua
- Sela aliandamwa na majuto kwa kuwa hakuwa na uhakika kuhusu mkondo ambao maisha yake yangechukua
- Kutokana na umaskini uliowakumba Kadogo alivalishwa matambara alipozaliwa
- Sela, Masazu na Kadogo wanaangamia wakati Sela na Masazu walipokwenda kumchukua Kadogo kwa kuwa hawangemudu utaratibu ufaao
- Mzee Butali alichanganyikiwa na kujawa na hasira kwa kuwa pesa alizomlipia Sela shuleni hazikuzaa matunda
***7 x 2 = 1 4***

**Damu Nyeusi**

**5.**

a) Samaki wa nehi za joto
Ukatili wa Peter kwa wafanyikazi wake Christine kuavya mimba Christian kujihusisha na mapenzi ya kiholela na Peter
Biashara haramu - ubadilishaji wa fedha Peter kuwapuja wavuvi Wazungu kujihusisha katika uasnerati
***4 x 1 = 4***

b) Damu Nyeusi
Dereva kukataa kumbeba Fikirini kwa vile ni mweusi

Fikirini kutozwa faini bure
Fikirini kuitiwa polisi kwa kutofunga zipu
Wanafunzi na mhadhili kumbagua
Fikirini kumwaibisha Fikirini kwa kumuamuru avue nguo zote na atoke akiwa uchi katikabaridi ***4 x 1 = 4***

c) Gilasi ya mwisho makaburini
Itikadi za ushirikina zilizozuia watu kutahadhari
Ukaidi wa vijana kama Semkwa na Josefina kukataa maonyo ya Msoi Vijana kujihusisha na anasa Wakora kuwaibia wateja na wahudumu wa baa la makaburini ***4 x 1 = 4***

d) Kikaza
Ufisadi wa Bw Mtajika Bw na Bi Mtaika kukaidi sheria za kikaza Baadhi ya wananchi kuwasaliti wanakijiji kama Bw Machupa
Wanakijiji kukosa uwajibikaji kwa kutojishughulisha na athari za chaguo lao la uongozi
Bwana Mtajika kuwadanganya wanakijiji kwa kuwapa ahadi za uongo *4 x 1 = 4*

e) Maeko
Unywaji wa pombe kupindukia
Duni kuwasumbua wanakijiji kwa nyimbo zake
Duni kumtesa Jamila
Ubinafsi - Salim kumshauri jamila amwache Duni amwoe yeye
Wanakijiji kutoa ushauri mbaya kwa Jamila ***4 x 1 = 4***

***hadithi zozote 5 x 4 = 20***

8. a)
i) Kitendawili ni kauli yenye fumbo ambalo hutolewa kwa hadhira hai ili ilifumbue ***alama 2***

ii)
- Kitangulizi cha kitendawili ainbacho hutolewa na mtegaji Mtegaji: Kitendawili
- Hadhira humpa ruhusa ya kutega: Mteguaji: Tega!
- Mtegaji hutoa kitendawili Mtegaji: Fatuma mchafu
- Jibu hutolewa na mteguaji Mteguaji: Nguruwe (kosa)
- Jibu likikosekana mtegaji huomba mji Mtegaji: Umenoa, nipe mji
- Mteguaji hutoa mji Mteguaji : Ninakupa Thika
- Mtegaji akipewa mji hutoa jawabu sahihi Mtegaji : Nilienda Thika, watu wa Thika wakaniambia nikija niwasalimu. Jibu lake ni fagio

***7x1***

b) i) Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee. Ni utumiaji wa lugha kwa mvuto na ufasaha *alama 2*

ii) <u>Sifa za ulumbi</u>
- Hutumia lugha kwa njia ya mvuto
- Hubainika katika muktadha wa kutoa hotuba
- Hutumia vipengele anuwai vya lugha kama vile sitiari, balagha, methali, nahau, taswira n.k
- Wa!umbi hutumiwa kuzungumza kwa niaba ya viongozi
- Walumbi hutumia chuku kwa ufanifu mkubwa
- Huwasilishwa kimantiki
- Huongozwa na utambuzi wa mazuri na mabaya katika jamii
- Huwa na lengo mahususi: kushauri, kutahadharisha ***5x1 = 5***

<u>Umuhimu wa ulumbi</u>
r) Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani
s) Hukuza ujuzi na ufasaha wa lugha
t) Ni msingi wa kuteua viongozi
u) Huhifadhi utamaduni wa jamii
v) Huburudisha
w) Hukuza uzalendo
x) Huweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu au ulio na athari kubwa
y) Ni kitambulisho cha utabaka ***4x1 = 4***